**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

# TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA WALIOFANYA MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA TATU MWAKA 2023

## 207 DINI YA KIISLAMU

Kimetayarishwa na

Baraza la Mitihani la Zanzibar

S. L. P. 3070,

Zanzibar.

©Baraza la Mitihani la Zanzibar, 2024

Haki zote zimehifadhiwa

## YALIYOMO

DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA ........ 1

3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI ........ 1

3.1.1 Swali la 1: Qur-ani ........ 1

3.1.2 Swali la 2: Qur-ani ........ 4

3.2.1 Swali la 3: Suna na Hadithi ........ 6

3.3.1 Swali la 4: Tawhidi ........ 9

3.3.2 Swali la 5: Tawhidi ........ 10

3.3.3 Swali la 6: Tawhidi ........ 12

3.3.4 Swali la 7: Tawhidi ........ 13

3.4.1 Swali la 8: Fiqhi ........ 15

3.4.2 Swali la 9: Fiqhi ........ 17

3.4.3 Swali la 10: Fiqhi ........ 18

3.4.4 Swali la 11: Fiqhi ........ 20

3.4.5 Swali la 12: Fiqhi ........ 21

3. 5. 1 Swali la 13: Tarekhe ........ 23

3.5.2 Swali la 14: Tarekhe ........ 26

3.5.3 Swali la 15 : Tarekhe ........ 30

4.0 HITIMISHO ........ 33

5.0 MAPENDEKEZO ........ 33

VIAMBATANISHO ........ 34

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Zanzibar limeandaa taarifa ya tathmini ya ufaulu wa watahiniwa wa mtihani wa kuingilia Kidato cha Tatu katika somo la Dini ya Kiislamu mwaka 2023. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu kwa wanafunzi, walimu, wazazi, waandaaji wa sera, watunga mitaala na jamii kwa ujumla kuhusu ufaulu wa watahiniwa kwa somo hilo.

Mtihani wa kuingilia Kidato cha Tatu ni mtihani ambao unakusudia kupima na kuona ni kwa namna gani watahiniwa wamejifunza kupitia miaka miwili ya Sekondari ya Awali. Kupitia matokeo ya mtihani huu, mtahiniwa hupokea matokeo hayo yanayomuonesha ufaulu kwa lengo la kuweza kuendelea na ngazi nyengine ya elimu au kutoendelea.

Uchambuzi uliyowasilishwa katika ripoti hii, unakusudia kuonesha sababu mbalimbali juu ya majibu ya watahiniwa katika somo la Dini. Ripoti inabainisha sababu tofauti zilizopelekea watahiniwa kujibu vizuri au vibaya. Miongoni mwa sababu za watahiniwa kufanya vizuri ni kufahamu matakwa ya swali, kufuata taratibu za uandishi hasa kwa maswali ya kuelezea na umaarufu wa baadhi ya mada kwa watahiniwa.

Aidha, watahiniwa walijibu vibaya kwa baadhi ya maswali kwa sababu zmbalimbali kama vil; kutofahamu malengo ya maswali hayo, watahiniwa kukosa ujuzi, maarifa juu ya baadhi ya maswali na kukosa mtiririko mzuri wa uandishi katika maswali ya kuelezea.

Vilevile, uchambuzi umeonesha vielelezo vya watahiniwa jinsi walivojibu vizuri au vibaya. Pia, uchambuzi huu umetumia jadweli ambazo zimebainishwa kwa rangi tofauti. Jadweli hizo hizo zinaonesha ufaulu wa watahiniwa hao kwa kila swali.

Kwa hiyo, ni imani ya Baraza kuwa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii yatachukuliwa na wadau wa elimu na kuyafanyia kazi kwa lengo la kuinua ufaulu wa somo la Dini katika mitihani yote inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Zanzibar linatoa shukurani kwa Maafisa Mitihani na wote walioshiriki katika kukamilisha Taarifa hii.

**Dkt. RASHID A. MUKKI**



**MKURUGENZI**

**BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

**ZANZIBAR**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua kiwango cha ufaulu wa mtihani wa kuingilia Kidato cha Tatu Kwa Somo la Dini Mwaka 2023. Mtihani ulitungwa kwa kuzingatia muhtasari wa Taifa wa mwaka 2010 na kufuata muundo wa mtihani wa Kidato cha Pili wa Baraza la Mitihani la Zanzibar wa mwaka 2015.

Mtihani huu ulikuwa na maswali kumi na tano (15) yaliyogawanywa katika sehemu A, B, C, D na E. Sehemu A, B, C na D yalikuwa ni maswali ya lazima ni sehemu ambazo watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu E ilikuwa na maswali matatu (3) ambapo mtahiniwa alitakiwa kuchagua maswali mawili.

## 2.0 SAMPULI YA WATAHINIWA

Idadi ya watahiniwa waliofanyiwa Tathmini ni **3,737** sawa na asimia **16.04** ya watahiniwa **23,296** waliosajiliwa kufanya mtihani wa somo hili. Uchambuzi kwa kila swali ulizingatia viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni vibaya, wastani na vizuri, ambapo vibaya ni kuanzia alama 0 hadi 29, wastani 30 hadi 64 na vizuri 65 hadi 100. Ufaulu huo umeoneshwa kupitia chati/grafu kwa kutumia rangi tatu ambazo ni: Kijani inawakilisha vizuri, manjano inawakilisha wastani na nyekundu inawakilisha vibaya.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

Sehemu hii, inaonesha maswali yaliyojibiwa na watahiniwa katika sehemu A, B, C, D na E. Pia inawakilisha asilimia ya watahiniwa waliojibu maswali pamoja na asilimia ya waliopata vibaya, wastani na vizuri. Mwisho, vielelezo vya watahiniwa waliojibu vizuri na vibaya vimeambatanishwa.

### 3.1 SEHEMU A: QUR-ANI

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili (2) yaliyotokana na mada ya Qur-ani, ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Swali la kwanza (1) lilikuwa na alama (12) na swali la pili (2) lilikuwa na alama (8). Hivyo jumla ya alama zote katika sehemu hii ni (20).

#### 3.1.1 Swali la 1: Qur-ani

Swali hili lilikuwa na vipengele vitatu (3) (a), (b) na (c) na kila kipengele kilichukua alama nne (4). Kipengele (a) cha swali kilimtaka mtahiniwa kukamilisha aya nne za suratul lahab, kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kutafsiri aya nne alizopewa na kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa kuandika mafunzo manne ya suratul lahab.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kusoma Qur-ani, kutafsiri pamoja na kutoa mafunzo.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,693** sawa na asilimia **98.82** na watahiniwa **44** sawa na asilimia **1.18** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 1a.


**Jadweli Nambari 1a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 3.5 | | 4 – 7.5 | | 8 - 12 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 938 | 25.40 | 1,374 | 37.20 | 1,381 | 37.40 | 2,755 | 74.60 |

Jadweli nambari 1a linaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **37.40** upo katika kiwango cha vizuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa mzuri kwa asilimia **74.60.**

Aidha watahiniwa **938** sawa na asilimia **25.40** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 1.1.

**Kielelezo 1.1 (kibaya)**


1. a) Kamilisha aya zifuatazo kwa hati za Kiarabu:

تَبَّتْ يَدَآ أَبِيْ لَهَبٍ وَّتَبَّ.

أ) Maa aghna anhu maaluhu wa makasbab

ب) Sayasla naaran dhata lahab

ج) Wamraatuhu hamalata lhatab

د) Fiijidiha hablun minmasad

b) Lete tafsiri ya aya zifuatazo kwa lugha ya Kiswahili.

أ) صِرَاطَ الَّذِيْنَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوْبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّيْنَ.

Njia ya wale waliokasirikiwa

Na shari ya aliyoumba

ج) لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُوْلَدْ.

Bwana wa viumbe wote

د) مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ.

Hao ni majini

c) Andika mafunzo manne (4) yanayopatikana katika Suratul-Lahab.

i. Tunajifunza ukweli

ii. Tunajifunza tumpende Allah

iii. Tuwe wakweli

iv. Tutakiane kheri kila wakati

Kielelezo nambari 1.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye ameshindwa kuandika Suratul Lahab kwa lugha ya Kiarabu. Pia ameshindwa kutoa mafunzo ya suratul lahab na kuandika mafunzo yasyoendana na swali husika.

Aidha, watahiniwa **1,381** sawa na asilimia **37.40** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 1.2

**Kielelezo (1.2) ( kizuri)**

1. a) Kamilisha aya zifuatazo kwa hati za Kiarabu:

تَبَّتْ يَدَآ أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ.

أ) مَآ أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُ وَمَا كَسَبَ

ب) سَيَصْلَىٰ نَارًا ذَاتَ لَهَبٍ.

ج) وَامْرَأَتُهُ حَمَّالَةَ الْحَطَبِ.

د) فِي جِيدِهَا حَبْلٌ مِنْ مَسَدٍ.

b) Lete tafsiri ya aya zifuatazo kwa lugha ya Kiswahili.

أ) صِرَاطَ الَّذِيْنَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوْبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّيْنَ.

Njia ya wale waliuneemeshewa juu yao, wala siwale waliaghadhibikiwa na wala si wale waliopotea.

ب) مِنْ شَرِّ الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ.

Mwenye kutia wasiwasi katika nyoyo za watu.

ج) لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُوْلَدْ.

Hakuzaa wala hakuzaliwa.

د) مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ.

Miongoni mwa Majini na watu.

c) Andika mafunzo manne (4) yanayopatikana katika Suratul-Lahab.

i. Tunatakiwa tusiwe ni wenye kutia fitina.

ii. Tufanye yale yaliamrishwa na Allah (S.W).

iii. Kuachana na matendo maovu.

iv. Siku ya mwisho utasaidiwa ni amali yako uliyoifanya

Kielelezo nambari 1.2 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali husika. Mtahiniwa huyu anaonekana alikuwa na ujuzi na maarifa ya kutosha juu ya mada ya Qur-ani na tafsiri yake kwa kuweza kujibu maswali aliyopewa katika vipengele vyote vitatu (3) kwa usahihi wake.

### 3.1.2 Swali la 2: Qur-ani

Swali hili lilikuwa na vipengele viwili (2) (a) na (b) na kila kipengele kilichukua alama nne (4). Kipengele (a) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutoa hukumu za usomaji wa Quran zinazohusiana na Nun Sakin na Tanwiin. Kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kufafanua mafunzo kwa ufupi yanayopatikana katika (106: 3).

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ujuzi na maarifa ya mtahiniwa katika kutoa hukumu za nuni sakina na tanwini pamoja na kuainisha ujumbe unaopatikana katika (106: 3).

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,695** sawa na asilimia **98.88**. Watahiniwa **42** sawa na asilimia **1.12** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 1b.


**Jadweli Nambari 1b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 2 | | 2.5 - 5 | | 5.5 - 8 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 756 | 20.46 | 1,646 | 44.55 | 1,293 | 34.99 | 2,939 | 79.54 |

Jadweli nambari 1b linaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **44.55** upo katika kiwango cha wastani, ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa mzuri kwa asilimia **79.54**.

Aidha watahiniwa **756** sawa na asilimia **20.46** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na ujuzi na maarifa ya kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 2.1.

**Kielelezo 2.1 (kibaya)**


2. a) Toa hukumu za usomaji wa Qur-an kwa tajwid unaohusiana na hukumu za nuni sakina na tanwin katika aya zifuatazo:

أ) نَفْسٌ بِمَا. Idigham
ب) وَأَنْذِرْهُمْ. Idiham kathira
ج) رُسُلًا مِنْ. Ikhfau
د) سَمِيعٌ عَلِيمٌ. Ikhfau.

b) "Basi muabuduni Bwana wa nyumba hii yaani Allah (S.W)" (106:3).


Ainisha ujumbe unaopatikana kwa waislamu kupitia aya hii.

Tumua bundu na kumshukuru Allah kwa kwenda kuhiji katika nyumba ya Allah (s.w) huko Maka.

Kielelezo nambari 2.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye ameshindwa kutoa hukumu za nuni sakina kwa usahihi wake pamoja na kutoa mafunzo yanayotokana na aya aliyopewa. Mtahiniwa huyu mfano katika kipengele cha kwanza alitakiwa kuandika hukumu ya ikhfau, badala yake ameandika id-gham.

Aidha watahiniwa **1,293** sawa na asilimia **34.99** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na ujuzi juu ya kile walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 2.2

**Kielelezo (2.2) ( kizuri)**


2. a) Toa hukumu za usomaji wa Qur-an kwa tajwid unaohusiana na hukumu za nuni sakina na tanwin katika aya zifuatazo:

أ) نَفْسٌ بِمَا. Hukmu ya Iq-lab.
ب) وَأَنْذِرْهُمْ. Hukmu ya Ikhfau.
ج) رُسُلًا مِنْ. Hukmu ya Id-gham
د) سَمِيعٌ عَلِيمٌ. Hukmu ya Idh-har.

b) "Basi muabuduni Bwana wa nyumba hii yaani Allah (S.W)" (106:3). Ainisha ujumbe unaopatikana kwa waislamu kupitia aya hii.

Hapana mola apasae kuabudiwa kwa hakki isipokuwa Allah (s.w). Haliyakuwa pekee Allah (s.w) hana mshirika, katika ibada zake wala katika ufalme wake.

Kielelezo namba (2.2) ni mfano wa mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili. Mtahiniwa anaonekana kuwa na ujuzi na maaarifa ya kutosha juu ya:

a) Kutoa hukumu za nuni sakina na tanwini.

b) Kuainisha ujumbe unaopatikana katika (106: 3).

**3.2 SEHEMU: B SUNNA NA HADITHI**

Sehemu hii ilikuwa na swali moja tu kutoka katika mada ya Sunna na Hadithi ambalo lilikuwa na alama kumi (10).

**3.2.1 Swali la 3: Suna na Hadithi**

Swali hili lilikuwa na vipengele kumi (10).Watahiniwa walitakiwa kuchagua jawabu sahihi kati ya jawabu walizopewa.

Kipengele cha (i) cha swali kilimtaka mtahiniwa kuainisha tafsiri sahihi ya hadithi maudhui kwa kuchagua katika jawabu zifuatazo:-

A. Ilio na uongo aliozuliwa Mtume (S.A.W)

B. Isio na sifa za hadithi sahihi

C. Wapokezi wake si waadilifu

D. Wapokezi wake si wenye udhibiti mkubwa

Kipengele cha (ii) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutaja kipindi ambacho wanazuoni wengi walipojitokeza kukusanya hadithi kwa kuchagua jawabu alizopewa ambazo ni:-

A. 3AH B. 4 AH C. 5 AH D. 6AH

Kipengele cha (iii) cha swali kilimtaka mtahiniwa kubainisha madaraja ya hadithi sahihi kulingana na jawabu alizopewa.

A. Iliyochambuliwa kwa masharti ya Tirmidhi na ibn Majah

B. Iliyokubaliwa na imamu Bukhari na imamu Muslim

C. Iliyopokelewa na Bukhari na Tirmidhiy

D. Wapokezi wake ni maarufu sana

Kipengele cha (iv) cha swali kilimtaka mtahiniwa kumtaja imamu mwenye kitabu cha Isnad bin Hambal katika jawabu alizopewa ambazo ni:-

A. Abdallah bin Hambal

B. Ahmad bin Hambal

C. Muhammad bin Hambal

D. Yahya bin Hambal

Kipengele cha (v) cha swali kilimtaka mtahiniwa kutaja idadi ya wanachuoni waliojitokeza kukusanya hadithi nyingi katika kipindi cha tabii tabiina, kama ifuatavyo:-

A. nne B. tano C. sita D. saba

Kipengele cha (vi) cha swali kilimtaka mtahiniwa kuainisha sehemu tatu zinazopelekea kukamilika kwa hadithi katika jawabu zifuatazo:-

A. Kuendelea kushuka Qur-ani kwa muda mrefu

B. Kutanuka kwa dola ya kiislamu

C. Kuwepo kwa masahaba waliohifadhi hadithi

D. Kuwepo kwa Mtume (S.A.W)

Kipengele cha (vii) cha swali kilimtaka mtahiniwa kueleza maana ya hadithi dhaifu kulingana na jawabu alizopewa.

A. Isnad, matin na masumulizi

B. Isnad, matin na rawi

C. Isnad, rawi na wapokezi

D. Matin, isnad na maelezo

Kipengele cha (viii) cha swali kilimtaka mtahiniwa kuainisha sababu zilizopelekea uandishi wa hadithi kuwa mdogo wakati wa Mtume (S.A.W) katika jawabu alizopewa kama ifuatavyo:-

A. Inafanana na hadithi sahihi bali wasimulizi wake ni dhaifu katika udhibiti

B. Miongoni mwa wasimulizi wake wanakasoro zilizojitokeza

C. Mtume (S.A.W) amezuliwa uongo katika aina hiyo ya hadithi

D. Wasimulizi wake ni wenye sifa zilizokamilika

Kipengele cha (ix) cha swali kilimtaka mtahiniwa ataje imamu aliyegawa hadithi katika matawi manne kwa kuchagua katika jawabu zifuatazo:-

A. Ibn Hajar B. Imamu Malik

C. Imamu Muslim D. Imamu Suyt

Kipengele cha (x) cha swali kilimtaka mtahiniwa kubainisha maana halisi ya kumfuata Mtume (S.A.W) kwa kuchaguwa katika jawabu alizopewa.

A. Kuhifadhi hadithi za Mtume (S.A.W) pamoja na kuzifanyia kazi

B. Kumfanyia wema Mtume (S.A.W) pamoja na masahaba wake

C. Kumsali Mtume (S.A.W) pamoja na kutukuza uzazi wake

D. Kumtii Mtume (S.A W) pamoja na kumfanya hakimu wa kila jambo

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima ufahamu na maarifa ya mtahiniwa katika kutoa ufafanuzi juu ya sunna na hadithi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,682** sawa na asilimia **98.53** watahiniwa **55** sawa na asilimia **1.47** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 2a.


**Jadweli Nambari 2a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 2.5 | | 3 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 931 | 25.28 | 2,457 | 66.74 | 294 | 7.98 | 2,751 | 74.72 |

Jadweli nambari 2a linaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **66.74** upo katika kiwango cha wastani ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa mzuri kwa asilimia **74.71**.

Aidha, watahiniwa **931** sawa na asilimia **25.28** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa hawakuwa na ufahamu wa kutosha juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 3.1.

**Kielelezo 3.1 (kibaya)**


JAWABU

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | D | B | C | D | C | C | D | C | B |

Kielelezo nambari 3.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali hili na badala yake aliweka herufi kwa kubahatisha mfano, (i) ameweka B badala ya A yenye kumaanisha (iliyo na uongo aliozuliwa Mtume (S.A.W).

Aidha watahiniwa **294** sawa na asilimia **7.98** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa hali hii inaonekana wazi katika kielelezo nambari 3.2

**Kielelezo (3.2) ( kizuri)**

JAWABU

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | A | B | B | C | D | B | B | D | D |

Kielelezo nambari 3.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi na kukosa kipengele ix, kipingele hichi usahihi wake ni A ikimaanisha Ibnu Hajar.

### 3.3 SEHEMU C: TAWHID

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) katika mada ya Tawhid. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali katika sehemu hii lilikuwa na alama tano (5) na kuifanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama ishirini (20).

#### 3.3.1 Swali la 4: Tawhidi

Swali la nne lilitokana na mada ya Tawhidi, ambapo mtahiniwa alitakiwa kuipanga kwa mpangilio wake mitume aliyopewa, ambayo ni:-

A. Nouh (A.S) kisha Hud (A.S)

B. Swaleh (A.S) kisha Ibrahim (A.S)

C. Adam (A.S) kisha Idrisa (A.S)

D. Is-hak (A.S kisha Yakub (A.S)

E. Lut (A.S) kisha Ismail (A.S)

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa na uelewa wa mtahiniwa juu ya kupanga mitume iliyotajwa ndani ya Qur-ani kwa mpangilio wake.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,681** sawa na asilimia **98.50** watahiniwa **56** sawa na asilimia **1.50** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 3a.

**Jadweli Nambari 3a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 1 | | 1.5 - 3 | | 3.5 5 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 491 | 13.34 | 574 | 15.59 | 2,616 | 71.07 | 3,190 | 86.66 |

Jadweli nambari 3a linaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **71.07** upo katika kiwango cha vizuri ambapo umepelekea ufaulu wa jumla kuwa mzuri kwa asilimia **86.61.**

Aidha, watahiniwa **491** sawa na asilimia **13.34** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na uelewa mzuri juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 4.1.

**Kielelezo 4.1 (kibaya)**

JAWABU

| i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|
| ii | iii | i | v | iv |

Kielelezo nambari 4.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye ameshindwa kufahamu maelekezo ya swali badala yake ameandika nambari za kirumi kwenye jawabu badala ya kuandika herufi.

Aidha, watahiniwa **2,616** sawa na asilimia **71.07** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na ufahamu juu ya kile walichoulizwa. Kielelezo nambari 4.2 kinaweka wazi hilo.

**Kielelezo (4.2) (Kielelezo kizuri)**

JAWABU

| i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|
| C | A | B | E | D |

Kielelezo nambari 4.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amefanikiwa kufahamu maelekezo ya swali na kuweza kujibu swali hili kwa usahihi, bila yakuandika nambari zake mwenywe. Hali inayoonesha kwamba alikuwa na uelewa mzuri juu ya mtiririko wa Mitume.

### 3.3.2 Swali la 5: Tawhidi

Swali la tano lilitokana na mada ya Tawhidi, ambapo mtahiniwa alitakiwa kubainisha namna nafasi ya fitrah inavyomsaidia mwanadamu katika kumjua Allah (S.W).

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa na ueledi wa mtahiniwa juu ya njia miongoni mwa njia za mja kumjua Mwenyezi Mungu ambayo ni nafasi ya fitrah.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,373** sawa na asilimia **90.26** watahiniwa **364** sawa na asilimia **9.74** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 3b.


**Jadweli Nambari 3b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 1 | | 1.5 - 3 | | 3.5 5 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,193 | 65.02 | 767 | 22.74 | 413 | 12.24 | 1,180 | 34.98 |

Jadweli nambari 3b linaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **65.02** upo katika kiwango cha vibaya. Hivyo ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa katika kiwango cha wastani kwa asilimia **34.98.**

Watahiniwa **2,193** sawa na asilimia **65.02** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na ujuzi mzuri juu ya mada waliyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 5.1.

**Kielelezo 5.1 (kibaya)**



5. Bainisha namna nafasi ya fitrah inavyomsaidia mwanadamu katika kumjua Allah (S.W).

i) Vipaji vya mwanaadamu
ii) Mazingira
iii) Nafsi ya fitra
iv) Wahyi
v) Nafasi ya mwanaadamu

Kielelezo nambari 5.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha nafasi ya fitrah inavyoweza kumsaidia mwanadamu katika kumjua Allah (S.W) na badala yake ametaja baadhi ya mambo ambayo yanayomuezesha mwanadamu kumjua Allah (S.W).

Aidha watahiniwa **413** sawa na asilimia **12.24** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na ujuzi na ueledi mzuri juu ya kile walichosmeshwa katika mada waliyotahiniwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 5.2

**Kielelezo (5.2) (Kielelezo kizuri)**


5. Bainisha namna nafasi ya fitrah inavyomsaidia mwanadamu katika kumjua Allah (S.W).

Namna nyesi ya fitrah inavyomsaidi mwanadamu katika kumjua allah ni
Fitrah ni uwezo wa mwanadamu kumjua Allah kwa sababu zifuatazo.
kwanza : Umbile lenyewe ni la kibinaadamu

Kielelezo nambari 5.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amejitahidi katika kubainisha namna nafasi ya fitrah inavyomsaisa mwanadamu katika kumtambua Mola wake aliyemuumba.

### 3.3.3 Swali la 6: Tawhidi

Swali la Sita lilitokana na mada ya Tawhidi, ambapo mtahiniwa alitakiwa kufafanua kwa kutoa dalili juu ya chanzo cha elimu katika Uislamu.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa na uelewa wa mtahiniwa juu ya kufafanua kwa kutoa dalili ndani ya Qur-ani kuhusiana na chanzo cha elimu katika Uislamu.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,530** sawa na asilimia **94.46** watahiniwa **205** sawa na asilimia **5.54** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 3c.


**Jadweli Nambari 3c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 1 | | 1.5 - 3 | | 3.5 5 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,080 | 58.93 | 672 | 19.04 | 778 | 22.03 | 1,450 | 41.07 |

Jadweli nambari 3c linaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **58.93** upo katika kiwango cha vibaya. Hivyo ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa katika kiwango cha wastani kwa asilimia **41.07**.

Watahiniwa **2,080** sawa na asilimia **58.93** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na uelewa mzuri juu ya mada husika waliyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 6.1.

**Kielelezo 6.1 (kibaya)**



6. Kwa kutoa dalili katika Qur-ani fafanua chanzo cha elimu katika Uislamu.

Chanzo cha elimu kimeanza toka mtume alikuwa akifanya mila za dini ya Babu yake Ibrahim pale alipokutana na malaika Jibril na kumtaka asome kwa jina la molawake aliye muumba . katika Suratul Alaq aya 1-5.

Kielelezo nambari 6.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyeeleza kuwa chanzo cha elimu kimetoka kwa Mtume (S.A.W) alipotakiwa asome na malaika Jibrilu.

Aidha, watahiniwa **778** sawa na asilimia **22.03** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa na uelewa mzuri juu ya walichosomeshwa kuhusiana na walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 6.2

**Kielelezo (6.2) (Kielelezo kizuri)**


6. Kwa kutoa dalili katika Qur-ani fafanua chanzo cha elimu katika Uislamu.

Chanzo cha elimu katika Uislamu ni Allah kwa Sababu Almungu amri ya mwanzo aliyoitoa kwa mwanaadamu ni kusoma "Soma kwa ajili ya Mola wako aliye kuumba" na alimfundisha Nabii Adam majina ya Vitu vyote.

Kielelezo nambari 6.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amejibu swali lake kwa usahihi. Mtahiniwa huyu ameweza kusema kuwa elimu mwanzo wake inatokana na Allah (S.W) pale alipomfundisha Nabii Adam (A.S) majina ya vitu vyote.

### 3.3.4 Swali la 7: Tawhidi

Swali la saba lilitokana na mada ya Tawhidi, ambapo mtahiniwa alitakiwa kuorodhesha sifa tano (5) anazotakiwa kuwa nazo muislamu.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa na ujuzi wa mtahiniwa juu ya sifa tano (5) anazotakiwa kuwa nazo muislamu.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,665** sawa na asilimia **98.07.** Watahiniwa **72** sawa na asilimia **1.93** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 3d.


**Jadweli Nambari 3d: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 1 | | 1.5 - 3 | | 3.5 - 5 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 410 | 11.18 | 308 | 8.41 | 2,947 | 80.41 | 3,255 | 88.82 |

Jadweli nambari 3d linaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **8.40** upo katika kiwango cha wastani. Hata hivyo ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa katika kiwango cha vizuri kwa asilimia **88.81.**

Watahiniwa **410** sawa na asilimia **11.18** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na maarifa mazuri juu ya mada iliyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 7.1.

**Kielelezo 7.1 (kibaya)**


7. Orodhesha sifa tano (5) anazotakiwa kuwa nazo Muislamu.

i. Kumuani Mwenye zimungu kuwa yupo

ii. Kuamini vitabu vyake na mitume yake.

iii. Kuamini siku ya muisho


iv. Kuwa mcha Mungu.

v. Kuamini shari na kheri zote zinazokana na Allah (S.W).

Kielelezo nambari 7.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyeorodhesha baadhi ya nguzo za imani na kuacha kuandika sifa za muislamu. Hali ambayo imepelekea mtahiniwa huyu kulikosa swali hili.

Aidha watahiniwa 2**,947** sawa na asilimia **80.40** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa na ujuzi mzuri juu ya kile walichosomeshwa kuhusiana na walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 7.2

**Kielelezo (7.2) (Kielelezo kizuri)**


7. Orodhesha sifa tano (5) anazotakiwa kuwa nazo Muislamu.

i. Awe mkeweli

ii. Awe muaminifu.

iii. Awe muadilifu.

iv. Awe mchamungu.

v. Ajikinge kutokana na maovu na machafu

Kielelezo nambari 7.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyelijibu vizuri swali hili. Hali hii inaonesha kuwa mtahiniwa huyu alikuwa na upambanuzi wa kutosha juu ya sifa za muislamu.

### 3.4 SEHEMU D: FIQHI

Sehemu hii ilikuwa na maswali ya kujaza mapengo katika nafasi zilizoachwa wazi kutoka katika mada ya Fiqhi. Sehemu hii ilikuwa ni ya lazima kwa watahiniwa wote na ilikuwa na maswali matano (5) ambapo kila swali lilikuwa na alama sita (6). Hivyo sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama (30).

#### 3.4.1 Swali la 8: Fiqhi

Swali hili lilitokana na mada ya fiqhi inayozungumzia mambo ya lazima anayotakiwa kufanyiwa maiti wa kiislamu. Swali hili lilikuwa na vipengele viwili (2) (a) na (b). Kipengele (a) cha swali kilimtaka mtahiniwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika kile anachotakiwa kufanyiwa maiti wa kiislamu mara tu baada ya kufa. Kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika maudhui inayohusiana na muislamu aliyekufa shahidi.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima matumizi na ufahamu wa mtahiniwa juu ya nini anatakiwa kufanyiwa maiti wa kiislamu pamoja na yule aliyekufa shahidi.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,672** sawa na asilimia **98.26**. Watahiniwa **65** sawa na asilimia **1.74** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 4a.


**Jadweli Nambari 4a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 1.5 | | 2 – 3.5 | | 4 - 6 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 600 | 16.34 | 593 | 16.15 | 2,479 | 67.51 | 3,072 | 83.66 |

Jadweli nambari 4a linaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **67.51** upo katika kiwango cha vizuri hali ambayo imepelekea ufaulu wa jumla kuwa katika kiwango cha vizuri kwa asilimia **83.66.**

**Watahiniwa 600 sawa na asilimia 16.34** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na ufahamu mzuri juu ya walichotahiniwa katika mada hiyo kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 8.1.


**Kielelezo 8.1 (kibaya)**


8. a) Mara tu mtu anapokufa anatakiwa aliyehai amrudishe mwili wake na amfumbe mikono yake taratibu.
b) Muislamu aliyekufa shahidi anafunikwa wala hachunguzwi bali atazikwa hivyo hivyo.

Kielelezo nambari 8.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa mzito wa ufahamu na ambaye hana uelewa kuhusiana na mambo anayatakiwa kufanyiwa maiti wa kiislamu.

Aidha watahiniwa **2,479** sawa na asilimia **67.51** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na uelewa mzuri kuhusiana na maiti wa kiislamu kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 8.2

**Kielelezo (8.2) (Kielelezo kizuri)**


8. a) Mara tu mtu anapokufa anatakiwa aliyehai amrudishe mdomo wake na amfumbe macho yake taratibu.
b) Muislamu aliyekufa shahidi haoshwi wala hasaliwi bali atazikwa hivyo hivyo.

Kielelezo nambari 8.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye alikuwa na uelewa mzuri juu ya mambo anayotakiwa kufanyiwa maiti wa kiislamu. Hali iliyopelekea kulijibu swali hili kwa usahihi.

### 3.4.2 Swali la 9: Fiqhi

Swali hili lilitokana na mada ya fiqhi inayozungumzia zaka na sadaka. Swali hili lilikuwa na vipengele viwili (2) (a) na (b). Kipengele (a) cha swali kilimtaka mtahiniwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuainisha nini sadaka. Kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika wanyama wanaostahiki kutolewa zaka.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa na ufahamu wa mtahiniwa juu ya zaka na sadaka.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,672** sawa na asilimia **98.26** watahiniwa **65** sawa na asilimia **1.74** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 4b.


**Jadweli Nambari 4b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 1.5 | | 2 – 3.5 | | 4 - 6 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 119 | 3.25 | 314 | 8.55 | 3,239 | 88.20 | 3,553 | 96.75 |

Jadweli nambari 4b linaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **96.75** upo katika kiwango cha vizuri hali ambayo imepelekea ufaulu wa jumla kuwa katika kiwango cha vizuri kwa asilimia **96.75.**

Watahiniwa **119** sawa na asilimia **3.25** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na ufahamu mzuri juu ya mada waliyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 9.1.

**Kielelezo 9.1 (kibaya)**


9. a) Sadaka ni Sunnah au huduma inayotolewa kwa mtu yoyote anayehitaji kwa ihsani bila ya kutarajia malipo yoyote kutoka kwake.


b) Aina za wanyama wanaostahiki kutolewa zaka ni punda, farasi, ngombe na twiga

Kielelezo nambari 9.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye ameshindwa kutoa maana ya sadaka kwa kutojaza kwa usahihi nafasi iliyoachwa wazi. Halikadhalika mtahiniwa huyu anaonekana kuwa na uwezo mdogo wa ufahamu juu ya mada ya zaka

na sadaka, hali ambayo imempelekea kushindwa kuorodhesha wanyama wanaostahiki kutolewa zakka.

Aidha, watahiniwa **3,239** sawa na asilimia **88.20** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa na ufahamu mzuri katika mada ya zaka na sadaka kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 9.2

**Kielelezo (9.2) (Kielelezo kizuri)**


9. a) Sadaka ni mali au huduma inayotolewa kwa mtu yoyote anayehitaji kwa ihsani bila ya kutarajia malipo yoyote kutoka kwake.

b) Aina za wanyama wanaostahiki kutolewa zaka ni Ng'ombe mbuzi, Kondoo na Ngamia

Kielelezo nambari 9.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa anayeonekana kuwa na utambuzi mzuri juu ya mada ya zaka na sadka, kiasi ambacho ameweza kukamilisha vizuri nafasi iliyoachwa wazi katika kukamilisha maana ya sadaka. Vile vile mtahiniwa huyu ameonesha utambuzi wake juu ya wanyama wanaostahiki kutolewa zaka kwa usahihi.

### 3.4.3 Swali la 10: Fiqhi

Swali hili lilitokana na mada ya fiqhi iayozungumzia kuchanganya sala. Swali hili likuwa na vipengele viwili (2) (a) na (b). Kipengele (a) cha swali kilimtaka mtahiniwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika jamuu taqdim. Kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kufafanua sababu zilizopelekea kuchanganya sala.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima matumizi na ufahamu wa mtahiniwa juu ya namna ya kuchanganya sala.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,513** sawa na asilimia **94.01**. Watahiniwa **224** sawa na asilimia **5.99** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 4c.


**Jadweli Nambari 4c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 1.5 | | 2 – 3.5 | | 4 - 6 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,265 | 64.47 | 803 | 22.86 | 445 | 12.67 | 1,248 | 35.53 |

Jadweli nambari 4c linaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **12.67** upo katika kiwango cha vizuri. Hali iliyopelekea ufaulu wa jumla kuwa katika kiwango cha wastanii wa asilimia **35.53.**

Watahiniwa **2,265** sawa na asilimia **64.47** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na ufahamu mzuri juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 10.1.

**Kielelezo 10.1 (kibaya)**



10. a) Jamuu taqdim ni aina ya taqdim ambayo hukusiana na ibada maalum.

b) Miongoni mwa sababu zinazompelekea Muislamu kuchanganya sala ni Kufuata taratibu na Kuacha kumuabudu Allah

Kielelezo nambari 10.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa taarifa juu ya jamuu taqdim na badala yake ametoa maelezo yasiyoendana na matakwa ya swali husika.

Aidha, watahiniwa **445** sawa na asilimia **12.67** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa na ufahamu mzuri kaika mada ya kuchanganya sala kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 10.2

**Kielelezo (10.2) (Kielelezo kizuri)**


10. a) Jamuu taqdim ni Kuchanganya swala kwa kutangulizwa kwa wepesi. swala.

b) Miongoni mwa sababu zinazompelekea Muislamu kuchanganya sala ni Msafiri na Mgonjwa

Kielelezo nambari 10.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejaribu kueleza vizuri maana ya jamuu taqdim pamoja na kutaja sababu stahiki zinazopelekea muislamu kuchanganya sala. Hali hii inanesha kuwa mtahiniwa huyu alikuwa pia na uwezo wa kuonesha namna ya ufanyikaji wa kuchanganya sala.

### 3.4.4 Swali la 11: Fiqhi

Swali hili lilitokana na mada ya fiqhi katika mada ya nguzo za kiislamu. Swali hili lilikuwa na vipengele viwili (2) (a) na (b). Kipengele (a) cha swali kilimtaka mtahiniwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kueleza maana ya shahada mbili. Kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika sifa ya yule anaesali lakini hasimamishi sala.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa na ufahamu wa mtahiniwa juu ya namna ya nguzo mbili za kiislamu, nazo ni shahada na kusimamisha sala.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,632** sawa na asilimia **97.19**. Watahiniwa **105** sawa na asilimia **2.81** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 4d.


**Jadweli Nambari 4d: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 1.5 | | 2 – 3.5 | | 4 - 6 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,188 | 32.71 | 1,535 | 42.27 | 909 | 25.02 | 2,444 | 67.29 |

Jadweli nambari 4d linaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **42.26** upo katika kiwango cha wastani. Hivyo imepelekea ufaulu wa jumla kuwa katika kiwango cha vizuri kwa asilimia **67.29.**

Watahiniwa **1,188** sawa na asilimia **32.71** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na ufahamu mzuri juu ya walichoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 11.1.

**Kielelezo 11.1 (kibaya)**


11. a) Maana ya shahada mbili ni Kitendo cha Kushahadia mara mbili kwa kusema 1) Ashhadu-Allailahaillalwa 2) Ashhaduanamuhamada rasuluwa Yani ni Kujielekeza kwa Allah (S.W)


b) Yule ambaye anaswali, lakini hasimamishi swala kwa mujibu wa Qurani huwa ni mwenye Kuswali bila ya kusimamisha Swala

Kielelezo nambari 11.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye hakuwa na maarifa mazuri juu ya maana ya shahada mbili pamoja na kutaja jina la yule anaye sali lakini

hasimamishi sala. Mtahiniwa huyu badala ya kuandika maana ya shahada, yeye kaandika maneno ya shahada kwa lugha ya Kiswahili. Hali hii inaonesha kuwa mtahiniwa huyu hakuwa na maarifa juu ya nguzo za kiislamu.

Aidha watahiniwa **909** sawa na asilimia **25.02** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa na ufahamu mzuri juu ya nguzo za kiislamu kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 11.2

**Kielelezo (11.2) (Kielelezo kizuri)**


11. a) Maana ya shahada mbili ni kushuhudia kuwa hapa Mola apasuwae kuabudiwa kwa haki isipo kuwa Allah na Muhammad s.w ni Mjumbe wa Allah.

b) Yule ambaye anaswali, lakini hasimamishi swala kwa mujibu wa Qurani huwa ni mwenye Kufanya Riyaa (Kujionesha)

Kielelezo nambari 11.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyekuwa na maarifa mazuri juu ya nguzo za kiislamu kwa kuweza kutoa maana ya shahada mbili kwa uwazi kabisa. Pia, mtahiniwa huyu ameweza kumtambua yule anayesali kwa kujionesha. Hii ni wazi kwamba mtahiniwa huyu ni mwenye kuzifanyia kazi nguzo hizo mbili za kiislamu.

### 3.4.5 Swali la 12: Fiqhi

Swali hili lilitokana na mada ya fiqhi katika mada ya nguzo za kiislamu. Swali hili lilikuwa na vipengele viwili (2) (a) na (b). Kipengele (a) cha swali kilimtaka mtahiniwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika sunna za sala. Kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kutoa maana ya unyenyekevu katika sala.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa na ujuzi wa mtahiniwa juu ya sunna za sala na kutoa ufafanuzi juu ya unyenyekevu katika sala.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **3,602** sawa na asilimia **96.38**. Watahiniwa **135** sawa na asilimia **3.62** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 4e.


**Jadweli Nambari 4e: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 1.5 | | 2 – 3.5 | | 4 - 6 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 2,278 | 63.25 | 884 | 24.54 | 440 | 12.21 | 1,324 | 36.75 |

Jadweli nambari 4e linaonesha watahiniwa waliopata kiwango cha wastani walikuwa ni asilimia ya ufaulu wa **24.54.** Hali iliyopelekea ufaulu wa jumla kuwa katika kiwango cha wastani wa asilimia **36.75.**

Watahiniwa **2,278** sawa na asilimia **63.25** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na ufahamu mzuri juu ya nguzo ya kiislamu ya sala kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 12.1.


**Kielelezo 12.1 (kibaya)**


12. a) Miongoni mwa sunna za swala ni Kutia udhu maskioni
Kupaka udhu mdomoni na Kuomba dua katika swala
b) Maana ya unyenyekevu katika swala ni kumnyenyekea
Mwenye-Enzi - Mungu kama kuamba
unamuona na unaimani juu yake yeye
na kile unachokipanya kwamba ipo siku
utalipwa juu ya hicho.

Kielelezo nambari 12.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyeshindwa kupambanua baina ya sunna za sala kama lilivyotaka swali na sunna za udhu katika kipengele (a), pia alishindwa kutoa maana ya unyenyekevu katika kipengele (b), na badala yake alijitahidi kwa kuandika maana yake ya unyenyekevu ambayo siyo sahihi.

Aidha watahiniwa **404** sawa na asilimia **12.21** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na maarifa na ufahamu mzuri juu ya nguzo za kiislamu kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 12.2

**Kielelezo (12.2) (Kielelezo kizuri)**


12. a) Miongoni mwa sunna za swala ni Atahiyatu ya mwanzo, kuombadua na kusoma suranyengine kama(Nasi)

b) Maana ya unyenyekevu katika swala ni Ni kujitulia kimwili kiakili na kifikra na kuzingatia nguzo zote za swala.

Kielelezo nambari 12.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amejibu vizuri swali hili katika vipengele vyote viwili. Hali inayoonesha kuwa mtahiniwa huyu alikuwa na uwezo mzuri wa kuitambua nguzo hiyo ya kiislamu.

## 3.5 SEHEMU E: TAREKHE

Hii ni sehemu inayohusiana na Tarekhe ya Kiislamu. Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu (3) ya kuelezea ambapo iliwataka watahiniwa kuchagua maswali mawili (2) tu. Kila swali lilikuwa na alama kumi (10). Hivyo sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 20.

### 3. 5. 1 Swali la 13: Tarekhe

Swali hili lilitokana na mada ya Tarekhe, ambapo mtahiniwa alitakiwa kueleza namna Mtume (S.A.W) alivyoandaa umma wa kiislamu Madina.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima uchambuzi wa mtahiniwa juu ya namna ya kuandaa umma wa kiislamu.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **1,898** sawa na asilimia **50.78**. Watahiniwa **1,839** sawa na asilimia **49.22** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 5a.

**Jadweli Nambari 5a: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 2.5 | | 3 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,575 | 82.99 | 278 | 14.64 | 45 | 2.37 | 323 | 17.01 |

Jadweli nambari 5a linaonesha kuwa asilimia kubwa ya ufaulu wa **82.99** upo katika kiwango cha vibaya. Hali iliyopelekea ufaulu wa jumla katika swali hili kuwa katika kiwango cha vibaya kwa asilimia **17.01**.

Watahiniwa **1,575** sawa na asilimia **82.99** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana kutokuwa na uchaguzi mzuri wa maswali katika sehemu hii kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 13.1.

**Kielelezo 13.1 (kibaya)**


13. Kwa kutoa hoja nne (4), elezea namna Mtume (S.A.W) alivyoandaa Umma wa Kiislamu Madina.

1) Mtume (S.A.W), alipigania uislam kwa jia ya kuwatusanya watu kidogo kidogo na kuwaelekeza jinsi uislamu ulivyo
2) Mtume (S.A.W). Alipohama maka na kuja madina kwa lengo la kusambaza uislam. Mtume (SAW) alipokuwa akiwaelekeza watu wa Madina dhidi ya uislam. Basi watu wa madina walianza kum rushia mawe na kumkashifu
3) Mtume (SAW) alipata watu wachache na kuanza kuwapa maelekeza dhidi ya uislamu na kumuelewa
4) Mtume (SAW). Alianza na hao watu wachache na hapo uislamu ukaanza kuenea katika nchi ya madina na watu wingi wa huko Madina walianza kuingia katika uislamu mmoja badala ya mwengine na hapo uislamu ukaenea nchini madina Mtume alipomaliza akaondoka ~~kat~~ katika nchi ya madina.

Kielelezo nambari 13.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa inayoonesha kuwa mtahiniwa huyu alijibu kwa kubahatisha katika swali hili na kupelekea kufanya vibaya.

Aidha watahiniwa **45** sawa na asilimia **2.37** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na uchaguzi na uchambuzi mzuri juu ya mada husika kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 13.2


**Kielelezo (13.2) (Kielelezo kizuri)**


13. Kwa kutoa hoja nne (4), elezea namna Mtume (S.A.W) alivyoandaa Umma wa Kiislamu Madina.

i) Alijenga msikiti: Msikiti wa madina ulijenda mara tu baada ya mtume kwenda madina ili kupanua na kukuza uislam

ii) Aliwaunganisha Aus na Hazraj: Madina kulikuwa na makabila mawili ambayo ni Aus na Hazraj yaliokuwa hayana umoja na wala hayashirikiani kwa chochote sio kiibada na wala kiuchumi. Baada ya mtume aliwaunganisha kwa pamoja na kujenga udugu.

iii) Alijenga Udugu: Mtume (S.A.W) alipokwenda madina aliondoka na maswahaba zake kuambatana pamoja kwenda madina na kuunganisha Udugu na watu wa madina ambao walikuwa muhajirina Answari na watu wa Makka ambao walikuwa


muhajirina na kuunganisha udugu
Aliwaanda wa kiimani. Aliwafundisha wote
kuwa na Imani ya kumwabudu Allah (S.W)
na kuweza kufanya chochote kwa
ajili ya Allah (s.w) pamoja na
dini ya kiislamu.

Kielelezo nambari 13.2 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa ambaye amejibu vizuri swali hili isipokuwa hoja yake ya mwisho mtahiniwa huyu ametoka nje ya alichoulizwa. Hii inaonesha kuwa mtahiniwa alikuwa na muelekeo mzuri juu ya alichoulizwa.

### 3.5.2 Swali la 14: Tarekhe

Swali la kumi na nne lilitokana na mada ya Tarekhe, ambapo mtahiniwa alitakiwa kufafanua mafunzo wanayopatikana waislamu wa leo kutokana na vitimbi vya Makkafiri wa Makka.

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa na matumizi aliyokuwanayo mtahiniwa kuhusiana na mada husika.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **2,814** sawa na asilimia **75.30**. Watahiniwa **923** sawa na asilimia **24.70** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 5b.

**Jadweli Nambari 5b: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 2.5 | | 3 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 1,037 | 36.86 | 981 | 34.86 | 796 | 28.28 | 1,777 | 63.14 |

Jadweli nambari 5b linaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **28.28** upo katika kiwango cha vizuri. Hali iliyopelekea ufaulu wa jumla katika swali hili kuwa katika kiwango cha wastanii wa asilimia **63.14.**

Watahiniwa **1,037** sawa na asilimia **36.86** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na maarifa mazuri juu ya mada iliyoulizwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 14.1.

**Kielelezo 14.1 (kibaya)**

14. Fafanua mafunzo manne (4) tunayoyapata waislamu wa leo kutokana na vitimbi vya makafiri wa Makka dhidi ya waislamu.

(i) Walitaka kumuua mtume (S.A.W) kwa uwezo wa Allah (S.W) walishindwa na kujitahidi na binu zao zote Mungu aliwawa akazifelisha mbinu zao za kutaka kumuua mtume

(ii) Walitaka kuwaua waislamu lakini Mungu

aliwapa adhabu na wakashindwa kuwaua waislamu walibaki kulalamika bila ~~kufa~~ kupata faida yoyote

(iii) Kila atakae silimu na kuwa ~~Mtu~~ muislamu walikuwa wakimuua waliona kwamba wakifanya hivyo uislamu utaondoka mjini mtume ~~S.W~~ (S.A.W)

aliwapa adhabu na wakashindwa kuwaua waislamu walibaki kulalamika bila ~~kufa~~ kupata faida yoyote

(iii) Kila atakae silimu na kuwa ~~Mtu~~ muislamu walikuwa wakimuua waliona kwamba wakifanya hivyo uislamu utaondoka mjini mtume ~~S.W~~ (S.A.W)


alipozidi kueneza uislamu na alifanikiwa kupata watu wingi kuwa waislamu

(iv) Makafiri walishinwa na nguvu baada ya kuona waislamu wanaengezeka kwa kiwango kikubwa walizidi kuwaua lakini bado waislamu wanaengezeka

Kielelezo nambari 12.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa mafunzo yanayotokana na vitimbi vya Makkafiri dhidi ya waisalmu Makka na badala yake ameeleza vitimbi vya Makkafiri dhidi ya waislamu. Hali hii inaonesha kuwa mtahiniwa huyu ameshindwa kupambanua baina ya mafunzo yanayopatikana katika vitimbi vya makafiri wa Makka na mafunzo yatokanayo.

Aidha, watahiniwa **796** sawa na asilimia **28.28** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na uwezo wa matumizi mazuri ya kufafanua kile kilichohitajika katika swali husika kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 14.2.

**Kielelezo (14.2) (Kielelezo kizuri)**



14. Fafanua mafunzo manne (4) tunayoyapata waislamu wa leo kutokana na vitimbi vya makafiri wa Makka dhidi ya waislamu.

Vitimbi vya makafiri wa Makka dhidi ya waislamu walikuwa wakiwatesa sana waislamu, kuwapiga na hata kuwanyima mahitaji yao. Yafuatayo ni Mafunzo tunayoyapata waislamu wa leo kutokana na vitimbi vya makafiri wa Makkah dhidi ya waislamu.

Tunajifunza kuwa muislamu hatakiwa awemetie dhidi ya mateso atakayo yapata kulingania dini ya Allah (S.w) Mfano mtume, makafiri walimkataa na walimdharau na hata kufikia kumtenga na kumnyima Mahitaji yao ya Muhimu mfano chakula n.k.

Tunajifunza kuwa tusimchelee yeyote yule katika kulingania dini ya Allah (S.w) wala tusikate tamaa, bali tuombe dua kwa Allah ili awaongoze katika upotofu wao na waweze kuongoze katika njia iliyo nyoofu hapa

ulimwenguni na akhera.

Tunajifunza kwa tuache familia zetu na nafsi zetu kwa ajili ya kupambana na vitimbi vya Makafiri Mfano Bibi Khadija ambaye alitumia akitoa mpaka mali zake kwa ajili ya kuitoa mbaa deni ya Allah (s.w).

ulimwenguni na akhera.

Tunajifunza kwa tuache familia zetu na nafsi zetu kwa ajili ya kupambana na vitimbi vya Makafiri Mfano Bibi Khadija ambaye alitumia akitoa mpaka mali zake kwa ajili ya kuitoa mbaa deni ya Allah (s.w).

Tunajifunza kuwa Nusra ya Allah na ushindi huja kwa kwa kushikamana kwa hati na uadilifu dhidi ya vitimbi vya makafiri. Mfano Muhammad (SA.W) alipashikamana na ukweli na uadilifu ndani yake.

Kwa hivyo Vitimbi vya Makafiri ni vikubwa na wanatumia mbinu mbali mbali katika kutaka kuondoa uislamu Mfano nji ya Israil kuwauwa watu wa palestina hivyo hatuna muda wowote dhidi ya kurudi mbele ya Allah (s.w) kwa kumuomba kwa imani thabit ili tuweze kufikisha lengo la

kuumbwa kwetu.

Kielelezo nambari 12.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili. Mtahiniwa huyu aliweza kutumia maarifa yake kutoa mafunzo yanayotokana na vitimbi vya Makkafiri wa Makka.

### 3.5.3 Swali la 15 : Tarekhe

Swali la kumi na tano lilitokana na mada ya Tarekhe, ambapo mtahiniwa alitakiwa kuchambua faida wanazopata waislamu kupitia maisha ya Nabii Adam (A.S).

Kwa ujumla swali hili lililenga kupima maarifa na matumizi aliyukuwanayo mtahiniwa kupitia ya Nabii Adam (A.S).

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa **2,238** sawa na asilimia **59.88**. Watahiwa **1,499** sawa na asilimia **40.12** hawakulijibu swali hili. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa unaonekana katika jadweli la 5c.


**Jadweli Nambari 5c: Uchambuzi wa Ufaulu wa Watahiniwa**

| UCHAMBUZI WA UFAULU | | | | | | UFAULU WA JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIBAYA | | WASTANI | | VIZURI | | | |
| 0 - 2.5 | | 3 - 6 | | 6.5 - 10 | | | |
| IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % | IDADI | % |
| 469 | 20.96 | 848 | 37.89 | 921 | 41.15 | 1,769 | 79.04 |

Jadweli nambari 5c linaonesha kuwa asilimia ndogo ya ufaulu wa **20.95** upo katika kiwango cha vibaya. Hali hii imefanya ufaulu wa jumla katika swali hili kuwa katika kiwango cha vizuri kwa asilimia **79.04**.

Watahiniwa **469** sawa na asilimia **20.96** wamepata ufaulu mbaya. Watahiniwa hawa wanaonekana hawakuwa na maarifa mazuri juu ya mada iliyotahiniwa kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 15.1

**Kielelezo 15.1 (kibaya)**


15. Chambua faida nne (4) wanazozipata waislamu kutokana na maisha ya Nabii Adam (A.S).

Faida ambazo Waislam tunazipata juu ya maisha ya Nabii Adam
- Elimu : Nabii adam alifundishwa vitu vingi na Allah (S.W.A) alipo kuwa peponi ambavyo Malaika walikuwa

- Maisha ya Nabii wetu Adam yalitufu...
ili

Kielelezo nambari 15.1 ni mfano wa karatasi ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili kwa kushindwa kufafanua faida zinazotokana na maisha ya Nabii Adam (A.S) na badala yake alikuja na maelezo kuhusiana na Nabii Adam (A.S).

Aidha, watahiniwa **921** sawa na asilimia **41.15** wamepata ufaulu mzuri. Watahiniwa hawa wanaonekana kuwa na kumbukumbu pamoja na matumizi mazuri juu ya kuleta uchambuzi katika mahitaji ya swali husika kama inavyoonekana katika kielelezo nambari 15.2


**Kielelezo (15.2) (Kielelezo kizuri)**

15. Chambua faida nne (4) wanazozipata waislamu kutokana na maisha ya Nabii Adam (A.S).

Nabii adam (a.s) : Ni nabii ambaye mwanzo wa maisha yake alikuwepo peponi lakini baada ya kula tunda ambalo aliambiwa asile naye akala basi allah (s.w) akamleta duniani yeye na hawa. zifuatazo ni faida wanazozipata waislamu kutokana na maisha ya nabii adam (a.s)

Tumepata kujifunza kwamba, tunatakiwa tujiepushe ushawishi wa Iblis : Kwani yeye ndiye ambaye alimshawishi nabii adam (a.s) aende aka chukue (akachume) tunda ambalo amekatazwa kuchuma.

Pia tumepata kujifunza kwamba hatuna budi Kuomba msamaha mara tu baada ya kutenda jambo ambalo ni kosa ; Kama ambavyo aliomba msamaha nabii adam (a.s).



Tuna takiwa tujiepushe na tabia za Iblis za kuchu kia viumbe wengine ambavyo havina hatia : kama ambavyo Iblis aliambiwa amsujudie adam (a.s) na aka kataa.

Pia tumepata faida ya kujua ~~nini chanzo~~ kwamba ~~cha kipo~~ allah (s.w) ana uwezo wa kutoa hukumu yeyote ambayo anaitaka yeye mwenye : kama ambavyo nabii adam alihukumiwa na allah (s.w) kwa

Pia tunatakiwa tusimchelee yeyote yule katika kulinga nia uislamu kwa muislamu yeyote : katika kipindi hichi kuna watu wengi ambao walijipanyea wababe lakini waislamu hatutakiwi kuwachelea watu kama hawa.

Kwa hivyo nivyema tukatambua kwamba maka firi walidharau kwa hatua mbali mbali katika kupinga uislamu lakini waislamu hawa ku kata tamaa na kuendelea na

Kielelezo 15.2 kinaonesha kuwa mtahiniwa alikuwa na maarifa na uelewa juu ya alichoulizwa kwa kuweza kuchambua faida tunazozipata kupitia maisha ya Nabii Adam (A.S). Hali inayoonesha kuwa mtahiniwa huyu alikuwa na ufahamu mzuri wa kufanyia kazi maisha ya Nabii Adam (A.S).

# 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa jumla wa ufaulu unaonesha kuwa maswali tisa yalijibiwa vizuri, maswali matano yalijibiwa wastani na swali moja lilijibiwa vibaya.

Katika uchambuzi huu umebaini matatizo mbalimbali yanayohitaji kutatuliwa kwa mfano, baadhi ya watahiniwa hawakuwa na ujuzi, maarifa, wala uweledi wa kuweza kukabiliana na mtihani huu.

Ambapo watahiniwa hao hawakufanya vizuri hasa katika mada ya shirki juu ya kutoa maana ya shirki na kutaja aina kuu nne za shirki. Pia katika mada ya hijja juu ya kueleza nguzo ya Hijja ambapo Hajji akiwacha hijja yake haitokubalika na arejee mwakani pamoja na kutaja aina kuu za tawafu kwa mpangilio wake.

Mwisho taarifa hii ya uchambuzi wa watahiniwa itawasaidia walimu na wanafunzi katika kuinua viwango vya ufaulu kwa somo hili la Dini ya kiislamu.

## 5.0 MAPENDEKEZO

- Somo la dini lipatiwe vitabu rejea.
- Walimu washajihishwe sana kulisomesha somo kwani linaonekana kupoteza hadhi yake.
- Walimu wawahamasishe wanafunzi juu ya umuhimu wa somo la Dini katika jamii yetu.
- Walimu wa Dini walisomeshe somo hili kwa moyo wao wote.
- Walimu wa somo wawe na utaratibu wa kukutana ili kujuwa changamoto zinazolikumba somo la Dini na kutafuta njia za kuzitatua.
- Pamoja na kwamba kila skuli kuna paneli ya somo la Dini, lakini ipo haja ya kuunda paneli kubwa itakayowashirikisha walimu wa maskuli tofauti ili kutatua changamoto zinazolikabili somo hili.
- Kadiri iwezekanavyo walimu wajitahidi kumaliza silibasi ya somo la Dini katika ufundishaji wao hali ya kuzingatia mafikio ya malengo mahususi.

## VIAMBATANISHO

## KIAMBATANISHO NAMBARI 1

UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA MWAKA 2023

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | FIQHI | 9 | 96.75 | VIZURI |
| 2 | TAWHIDI | 7 | 88.82 | VIZURI |
| 3 | TAWHIDI | 4 | 86.66 | VIZURI |
| 4 | FIQHI | 8 | 83.66 | VIZURI |
| 5 | QURAN | 2 | 79.54 | VIZURI |
| 6 | TAREKHE | 15 | 79.04 | VIZURI |
| 7 | SUNNA NA HADITHI | 3 | 74.71 | VIZURI |
| 8 | QURAN | 1 | 74.60 | VIZURI |
| 9 | FIQHI | 11 | 67.29 | VIZURI |
| 10 | TAREKHE | 14 | 63.14 | WASTANI |
| 11 | TAWHIDI | 6 | 41.07 | WASTANI |
| 12 | FIQHI | 12 | 36.76 | WASTANI |
| 13 | FIQHI | 10 | 35.53 | WASTANI |
| 14 | TAWHIDI | 5 | 34.98 | WASTANI |
| 15 | TAREKHE | 13 | 17.01 | VIBAYA |

**KIAMBATANISHO NAMBARI 2**

UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI NA MADA
MWAKA 2022

| S/N: | MADA | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | TAWHIDI | 3 | 84.67 | VIZURI |
| 2 | FIQHI | 9 | 81.65 | VIZURI |
| 3 | TAREKHE | 13 | 71.27 | VIZURI |
| 4 | TAWHIDI | 4 | 65.86 | VIZURI |
| 5 | TAWHIDI | 7 | 63.76 | WASTANI |
| 6 | FIQHI | 12 | 62.51 | WASTANI |
| 7 | TAREKHE | 15 | 62.00 | WASTANI |
| 8 | FIQHI | 8 | 61.34 | WASTANI |
| 9 | FIQHI | 10 | 59.57 | WASTANI |
| 10 | FIQHI | 11 | 58.53 | WASTANI |
| 11 | TAWHIDI | 6 | 56.68 | WASTANI |
| 12 | QURAN | 2 | 55.09 | WASTANI |
| 13 | QURAN | 1 | 49.91 | WASTANI |
| 14 | TAREKHE | 14 | 45.67 | WASTANI |
| 15 | TAWHIDI | 5 | 11.02 | VIBAYA |